Nuru ya Kiswahili, Juzuu 4(2), Desemba 2025:49-73
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru42.4973

Tathmini ya Tafsiri ya Majina ya Pekee ya Watu kutoka Kiswahili kwenda Gịrịmi: Mifano kutoka *Agano Jipya*

Rehema Stephano
Profesa Mshiriki, Chuo Kikuu cha Dodoma
rehema.stephano2@udom.ac.tz
https://orcid.org/0000-0002-7277-9733

Ikisiri

Tafsiri ni muhimu sana kwa sababu inaunganisha watu wanaozungumza lugha tofauti. Majina ya pekee ya watu ni kipengele muhimu pia cha kutafsiriwa kwa sababu humbainisha mwenye jina na kuwasilisha ujumbe unaobebwa na mwenye jina hilo. Makala hii inatathmini tafsiri ya majina ya pekee ya watu kutoka *Agano Jipya la Kiswahili* kwenda *Agano Jipya kwa Gịrịmi*. Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano imetumika katika tathmini hiyo. Data zilizotumika kwenye makala hii zimekusanywa kwa njia ya uchambuzi matini na usaili. Makala inaonesha kwamba mikakati inayotumika kutafsiri majina katika matini teule ni miwili ambayo ni unakilishaji na utohozi wa majina. Hata hivyo, unakilishaji sauti una dosari kadhaa kwa sababu ya kuhamishia fonolojia na mofolojia ya Kiswahili katika Gịrịmi. Pia, kuna upungufu katika tafsiri ya majina hayo ambao unatokana na kubadilishwa kwa sauti kusikotabirika, tafsiri kuegemea zaidi katika Kiingereza badala ya Kiswahili ambayo ni matini chanzi mama, na kukosekana kwa urari katika kutafsiri jina moja. Makala hii inapendekeza tafsiri ya majina ya pekee ya watu kutoka lugha moja kwenda nyingine kufanyika kwa usahihi na urari ili dhima inayobebwa na majina hayo iweze kuakisiwa katika matini lengwa.

Dhana za Msingi: Tafsiri, majina ya pekee, Gịrịmi, *Agano Jipya*

Utangulizi

Majina, hususani ya pekee, kama kipengele kimojawapo cha lugha, hubeba taarifa, maarifa, ujumbe na hisia maalumu za lugha mahususi. Binadamu

hutoa majina kwa kila kitu kwa lengo la kutambulisha na kurahisisha mawasiliano (Okal, 2012). Majina ya pekee wanayopewa watu ni utambulisho na ubainisho unaomtofautisha mwenye jina na watu wengine. Kwa hiyo, jina ni sehemu muhimu ya maisha. Majina ya pekee ni nyeti sana kwa sababu huwakilisha uhusiano wa mwenye jina na historia yake (Naumova, 2014). Jina la pekee lina dhima mbalimbali kama vile kuwakilisha upekee wa mhusika na utambulisho wa kijamii. Wakati mwingine, jina ni urithi wa familia kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Kwa kusikia tu jina, mtu anaweza kubashiri asili au mahali alikozaliwa na anakotokea mwenye jina. Vilevile, jina huweza kuwakilisha hadhi ya kijamii ya mhusika.

Kutokana na dhima hizo muhimu, ni lazima majina ya pekee yahawilishwe kutoka lugha moja kwenda nyingine. Majina ya pekee hutafsiriwa ili watumiaji wa LL waweze kupata ujumbe unaoambatana na majina hayo. Hata hivyo, kuhawilisha majina ya pekee si kazi nyepesi (Okal, 2012; Valixon, 2020). Ugumu wa kuhawilisha majina hayo husababishwa na masuala makubwa manne. Mosi, ni tofauti za kiisimu, ambapo kila lugha ina sauti na maumbo tofauti na nyingine (Halimal, 2016). Pili, ni tofauti za kitamaduni, kijamii na kimazingira baina ya jamii yalikoundiwa majina hayo na jamii ya wanaotafsiriwa matini (Naumova, 2014; Shirinzadeh na Mahadi, 2014). Tatu, majina ya pekee, yaliyo mengi, hayana visawe vya moja kwa moja katika LL kwa sababu, mara nyingi, huundiwa katika jamii fulani mahususi (Dweik na Al-Sayyed, 2016; Aubakir na Makhpirov, 2019). Nne, ugumu wa tafsiri za majina ya pekee, hasa katika matini za kidini, husababishwa na wafasiri kukosa uelewa au maarifa ya kitaalamu ya kidini yanayoambatana na majina hayo.

Kwa mantiki hiyo, tafsiri ya majina ya pekee inahitaji umakini wa kipekee kwa sababu dosari zozote zinazohusiana na tafsiri ya majina hayo zinaweza kusababisha upotoshaji na tafsiri ya matini lengwa (ML) kutoeleweka (Aubakir na Makhpirov, 2019). Upotoshaji wa tafsiri ya majina ya pekee hupoteza maana ya majina na ujumbe kwa ujumla na kusababisha matini kukosa thamani kutokana na makosa yaliyomo katika matini hiyo (Issa, 2017). Kwa hiyo, tafsiri ya majina ya pekee inabidi ifanywe kwa tahadhari kubwa kwa kuzingatia kanuni mwafaka ambazo haziwezi kufifisha wala kupotosha ujumbe wa matini chanzi (MC) (Okal, 2012). Kwa hali hiyo, mfasiri wa majina ya pekee hapaswi kuwa na maarifa ya kiisimu tu, bali pia maarifa mahususi ya kimazingira na kitamaduni ya majina anayoyashughulikia; la sivyo, atawapotosha wasomaji wa ML (Aubakir na Makhpirov, 2019).

Kutokana na thamani na umuhimu wa majina, utafiti umefanyika ili kutathmini mikakati iliyotumika na upungufu uliojitokeza katika kutafsiri majina ya pekee ya watu kutoka *Agano Jipya* kwa Kiswahili kwenda Gɪrɪ̣mi[1]. Tathmini hii inalenga kuboresha tafsiri za majina ya pekee ya watu katika matini mbalimbali ili kufanikisha kusudi kuu la tafsiri ambalo ni mawasiliano.

Nadharia ya Utafiti

Nadharia ya Ulinganifu wa Mawasiliano ya Eugine Nida (1969) imeongoza uchambuzi wa data za makala hii. Nadharia hii inadai kwamba, katika

[1] Gɪrɪ̣mi(F32)—kwa matamshi ya Kiswahili Kirimi)—ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa Mkoa wa Singida, nchini Tanzania. Lugha hii ina lahaja tatu: *Gɪ̣irwana* (Kiirwana) inayozungumzwa Tarafa ya Mtinko na ya Ilongero, Wilayani Singida; *Gɪnyamụnying'anyi* (Kinyamnying'anyi) inayozungumzwa Tarafa ya Mgori, Wilayani Singida na Gɪ̣ahi/Chahi (Kiahi/Chahi) inayozungumzwa eneo lote la Wilaya ya Ikungi. Wazungumzaji wa lugha hii wanajulikana kwa jina la *Arɪ̣mi* na wazungumzaji wa lahaja zake hujulikana kama *V*(*a*)*irwana*, *Anyamụnying'anyi* na *Va*(*a*)*hi*, kwa mfuatano huo. Lakabu ya Gɪrɪ̣mi ni Gɪnyaṭụ(r)ụ (Kinyaturu).

tafsiri, vipengele vinavyohawilishwa ni lazima vifanane au vikaribiane na vya LL. Lengo ni kuwa na uasili timilifu wa LL katika sarufi, msamiati na utamaduni. Ujumbe wa LC na LL ni lazima ueleweke kwa namna moja kwa wasomaji wa MC na ML. Nadharia hii imetumika kwa sababu inaonekana ndiyo bora kutafsiri matini za kidini ikilinganishwa na nadharia zingine. Nichols (1996), mathalani, anadai kuwa, kabla ya karne ya 20, tafsiri za kidini, kwa kiasi kikubwa, zilifanyika kwa kutumia Nadharia ya Ulinganifu wa kimuundo. Tafsiri hizo hazikusomeka wala kueleweka kwa urahisi kwa wasomaji wa ML kwa sababu zilifanyika kisisisi. Kwa hiyo, zilisomeka kigeni. Baada ya kuanzishwa kwa Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano, tafsiri za matini za kidini, hasa za *Agano Jipya*, zilianza kueleweka.

Methodolojia

Mbinu mbili za utafiti zimetumika kukusanya data za ambazo ni uchambuzi matini na usaili. Matini na watafitiwa wote waliosaliwa walipatikana kwa usampulishaji lengwa. Matini zilizochambuliwa ni *Agano Jipya* na tafsiri yake ya Gịrịmi *(Iraghano në Ifya gwa Antu Voong'e gwa Murighëëtyo wa Gërëmi*). Usaili ulihusisha watafitiwa wa makundi mawili. Mosi ni wafasiri 4 wa *Agano Jipya* kwa Gịrịmi. Hawa walihusishwa kwa sababu walifanya tafsiri teule, hivyo, walitarajiwa kuwa na uelewa mpana kuhusu mchakato wa tafsiri, hasa ya matini teule. Pili ni wazungumzaji wazawa 4 wa Gịrịmi wazaliwa wa Kijiji cha Mwakichenche wenye umri kati ya miaka 40 na kuendelea ambao wanafahamu Kiswahili pia.

Mikakati Iliyotumika Kutafsiri Majina ya Pekee ya Watu

Tathmini iliyofanyika imeonesha kuwa kuna mikakati mikubwa miwili inayotumika kutafsiri majina ya pekee ya watu kutoka Kiswahili kwenda Gịrịmi. Mikakati hiyo ni unakilishaji wa majina na utohoaji wa majina.

Unakilishaji wa majina

Utafiti ulibaini kwamba kuna majina ya pekee ya watu yanayohamishwa kama yalivyo—bila maboresho yoyote—kutoka Kiswahili kwenda Gịrịmi. Mkakati wa unakilishaji wa majina unaongoza kutafsiria majina hayo kuliko utohoaji. Data Na. 1 imebeba majina yaliyohawilishwa katika Gịrịmi kwa kutumia unakilishaji.

Data Na. 1

Matayo - Matayo	Yose - Yose	Isaka - Isaka
Daudi - Daudi (Dụdi)	Yohana - Yohana	Sauli - Sauli
Tamari - Tamari	Timayo - Timayo	Ainea - Ainea
Rahabu - Rahabu	Mariamu - Mariamu	Roda - Roda
Obedi - Obedi	Elisabeti - Elisabeti	Nigeri - Nigeri
Uria - Uria	Gabrieli - Gabrieli (Gabureri)	Serigio - Serigio
Abiya - Abiya	Fanueli - Fanueli	Androniko - Androniko
Asa - Asa	Mathati - Mathati	Yunia - Yunia
Yoramu - Yoramu	Lawi - Lawi	Urbano - Arbano
Manase - Manase	Matathia - Matathia	Aristobulo - Aristobulo
Yosia - Yosia	Amosi - Amosi	Narkiso - Narkiso
Yekonia - Yekonia	Nahumu - Nahumu	Rufo - Rufo
Abihudi - Abihudi	Nagai - Nagai	Herme - Herme
Eliakimu - Eliakimu	Maathi - Maathi	Herma - Herma
Sadoki - Sadoki	Semei - Semei	Filologo - Filologo
Akimu - Akimu	Elima - Elima	Yulia - Yulia
Eliudi - Eliudi	Kishi - Kishi	Nerea - Nerea
Eleasari - Eleasari	Timoteo - Timoteo	Olimpa - Olimpa
Yakobo - Yakobo	Sila - Sila	Lukio - Lukio
Herode - Herode	Zeu - Zeu	Yasoni - Yasoni
Yuda - Yuda	Lidia - Lidia	Teritio - Teritio
Arikelao - Arikelao	Galio - Galio	Stefana - Stefana
Musa - Musa	Akila - Akila	Kefa - Kefa
Eliya - Eliya	Gayo - Gayo	Akaiko - Akaiko
Herodia - Herodia	Sekundo - Sekundo	Areta - Areta
Danieli - Danieli	Eutiko - Eutiko	Hajiri - Hajiri
Yeremia - Yeremia	Agabo - Agabo	Euodia - Euodia
Resa - Resa	Teritulo - Teritulo	Sintike - Sintike
Kosamu - Kosamu	Anania - Anania	Onesimo - Onesimo
Adamu - Adamu		Tikiko - Tikiko

Yorimu - Yorimu Melea - Melea Mena - Mena Yese - Yese Boazi - Boazi Lameki - Lameki Shemu - Shemu Yaredi - Yaredi Mahalaleli - Mahalaleli Elisha - Elisha Yoana - Yoana Susana - Susana Yairo - Yairo Samsoni - Samsoni Gadi - Gadi	Yulio - Yulio Sara - Sara Isaya - Isaya Baali - Baali Kayafa - Kayafa Anasi - Anasi Nikodemo - Nikodemo Baraba - Baraba Samweli - Samweli Safira - Safira Gamalieli - Gamalieli Nikanori - Nikanori Fa Simeoni - Simeoni Abadoni - Abadoni rao - Farao Tito - Tito	Dema - Dema Luka - Luka Himenayo - Himenayo Loisi - Loisi Eunike - Eunike Figelo - Figelo Onesiforo - Onesiforo Fileto - Fileto Eubulo - Eubula Afia - Afia Kaini - Kaini Esau - Esau Filimoni - Filimoni Gideoni - Gideoni (Gidioni) Mikaeli - Mikaeli (Mikeli)

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Katika Data Na. 1, tunaona majina ya pekee ya watu yamehamishwa kama yalivyo katika LL ambayo ni Gɪrɪ̣mi. Unakilishaji ni mkakati unaotumika zaidi kutafsiri majina ya pekee ya watu kuliko mikakati mingine, ambapo mfasiri huhamisha majina ya LC kama yalivyo kwenye LL bila kubadilisha chochote (Shirinzadeh & Mahadi, 2014; Kishe, 2016; Valixon, 2020). Wataalamu wanaeleza faida kuu mbili za mkakati huu. Mosi, ML inakuwa na ufanano mkubwa na MC yake kwa sababu majina hayatafsiriwi bali yanahamishwa. Pili, ML inahifadhi utamaduni chasili. Kishe (2016) anadai kuwa majina yanayohamishwa huendana na maumbo ya LL. Anaongeza kwamba tafsiri ya aina hii ni rahisi tofauti na ile inayozingatia matamshi ya LC.

Hata hivyo, kupitia usaili, imeonekana kuwa baadhi ya majina yamenakiliwa kwa makosa. Msailiwa mmoja aitwaye Makita[2] alisema, "Jina *Yesu*, kwa mfano, lilipaswa kuwa *Yesụ* kwa sababu matamshi yake katika Gịrịmi hutumia /ụ/ ambayo ni irabu ya juu, kati, nyuma". Kutumia irabu, /u/, kwa mujibu wa Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano, ni ukiukaji wa matamshi sahihi na upunjaji wa ladha halisi ya matamshi ya Gịrịmi.

Kadhalika, baadhi ya majina yamenakiliwa yakiwa na mkururo wa konsonanti badala ya kuwa na silabi huru ambalo ni hitaji la msingi la lugha za Kibantu. Majina hayo yalipaswa kutoholewa kwa kuchopekwa irabu katikati ya mikururo hiyo ili kuunda silabi huru kulingana na matakwa ya sarufi ya LL. Mifano ifuatayo ya majina kama ilivyowasilishwa katika Data Na. 1 inaonesha mkururo wa konsonanti katika majina teule.

Gabrieli - Gabrieli (Gabureri)
Androniko - Androniko
Urbano - Arbano
Narkiso - Narkiso
Herme - Herme
Herma - Herma
Stefana - Stefana

Majina haya yalipaswa kutoholewa, yaani kuzingatia fonolojia na mofolojia ya Gịrịmi. Mjadala zaidi kuhusu utohozi, hasa wa kuchopeka irabu utafanyika katika kipengele kinachohusu uchopekaji wa irabu.

Aidha, katika tafsiri ya *Agano Jipya* la Kiswahili kwenda Gịrịmi, baadhi ya majina yametafsiriwa kwa sauti ambazo hazipo katika Gịrịmi. Majina haya

---

[2] Mahojiano baina ya mtafiti na Anna Makita yalifanyika tarehe 12/09/2023 katika Kijiji kilichotajwa.

yangeweza kupewa sauti ambazo zipo katika lugha pokezi ili yawe na uasili katika utamkaji. Ifuatayo ni mifano ya majina hayo ya pekee kama yalivyowasilishwa katika Data Na. 1 iliyotangulia.

Ma**th**ati - Ma**th**ati
Mata**th**ia - Mata**th**ia
Maa**th**i - Maa**th**i
Boa**z**i - Boa**z**i
Shemu - **Sh**emu
Eli**sh**a - Eli**sh**a
Ki**sh**i - Ki**sh**i
Zeu - **Z**eu

Sauti /ɵ/, /ʃ/ na /z/ zilizotumika katika baadhi ya maneno yaliyomo katika Data Na. 1 hazipo katika Gɪṛṃi. Tafsiri ya majina yenye sauti /ɵ/ ingeweza kutumia sauti /t/ kama ilivyofanyika katika majina yaliyowasilishwa katika Data Na. 5. Vilevile, majina yenye sauti /ʃ/ na /z/ yangeweza kutumia sauti /s/ kama ilivyowasilishwa katika Data Na. 6 na Na. 7. Kwa upande mwingine, uhamishaji huu wa sauti katika Kiswahili unaweza kuwa mwanzo wa kuingiza sauti mpya katika Gɪṛṃi. Winford (2003) anaeleza kuwa, wakati mwingine, ukopaji huingiza sauti mpya katika LL. Katika usaili, ilionekana kwamba sauti /ʃ/ na /z/, kwa sasa, zinatumiwa na baadhi ya wazungumzaji wa Gɪṛṃi. Akithibitisha hoja hii, Mnyawi[3] anasema:

> Siku hizi baadhi ya watu wanaweza kutamka majina kama vile Shabani, Shamimu, Shaila, Zawadi na Riziki ambayo zamani (hata sasa kwa baadhi ya watu, hasa wazee) yalikuwa yakitamkwa Sabani, Samimu, Saila, Sawadi na Risiki, kwa mfuatano huo.

Kwa ushuhuda huu, ni dhahiri kuwa sauti hizi zimeshaanza kuingia katika Gɪṛṃi na zinatumika. Ili kuepuka uradidi, mjadala zaidi kuhusu ubadilishaji

[3]Mahojiano baina ya Samweli Mnyawi na mtafiti yalifanyika tarehe 12/09/2023 katika Kijiji kilichotajwa.

wa sauti katika tafsiri utafanyika katika kipengele kinachohusu ubadilishaji wa sauti za konsonanti.

Utohoaji wa majina

Utohoaji wa majina unahusu kukopa neno la LC na kuliboresha kwendana na fonolojia na mofolojia ya LL. Mkakati huu unatajwa kufaa kutafsiria majina ya pekee kwa sababu, kwa kiasi kikubwa, huhifadhi muundo wa neno wa LC pamoja na dhima yake. Tulibaini kuwa utohoaji umefanyika kwa kutumia mikakati midogo mitatu ambayo ni ubadilishaji wa sauti, uongezaji wa sauti, na udondoshaji wa sauti. Mikakati hiyo midogo imeweza kutumika zaidi ya moja kutafsiri jina moja, jambo linaloelezwa pia na Msuya & Mreta (2019).

Ubadilishaji wa sauti

Ubadilishaji wa sauti unahusu kuondoa sauti ya LC na kuweka sauti inayopatikana au kuzoeleka katika LL. Katika tafsiri ya majina ya pekee ya watu kutoka Kiswahili kwenda Gịrịmi, ubadilishaji wa sauti unajumuisha sauti za irabu na za konsonanti. Ubadilishaji wa irabu umehusisha majina machache sana ikilinganishwa na ubadilishaji wa konsonanti. Data Na. 2 inaonesha mabadiliko hayo.

Data Na. 2

Eli**e**zeri - Eli**a**zeri Mana**e**ni - Mana**a**ni	Kl**e**opa - Kil**i**opa Sim**e**oni - Sim**i**oni	Prokon**o** - Furokon**i** Henok**o** - Henok**i**

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Data Na. 2 inaonesha mabadiliko ya irabu /e/ kuwa /a/ au /i/, na irabu /o/ kuwa /i/. Hata hivyo, kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika, mifano inayohusu mabadiliko hayo ni michache sana. Uchache huu wa mifano

hautoi ithibati ya kutosha kuhitimisha kwamba mabadiliko hayo yanafanyika kwa namna hiyo kutoka Kiswahili kwenda Gịrịmi.

Aidha, sauti za konsonanti za Kiswahili /p/, /ɵ/, /ɟ/ zimebadilishwa kwa sauti /f/, /t/, na /j/, na sauti /z/ na /ʃ/ zimebadilishwa kwa /s/, kwa mfuatano huo. Sauti za LC zimebadilishwa kwa sauti zinazopatikana, zilizozoeleka au kwendana na mazingira ya utokeaji wa sauti hizo katika maneno ya LL. Utafiti umeonesha zaidi kuwa, katika tafsiri ya majina ya watu, kuna sauti za Kiswahili zinazobadilishwa kwa sauti za Gịrịmi ingawa sauti hizo za Kiswahili zipo katika Gịrịmi pia. Sauti /p/ inabadilishwa kutoka Kiswahili kwenda Gịrịmi kwa sauti /f/ kwa sababu za mazingira ya utokeaji wa sauti hizo, na sauti /ɟ/ inabadilishwa kwa /j/ kwa sababu za upendeleo wa kutumia /j/ katika Gịrịmi kuliko /ɟ/. Data Na. 3 na 4 zinaonesha mabadiliko hayo.

Data Na. 3

Peresi - **F**aresi	**P**aulo - **F**aulo (Fulo)	Am**p**liato - Am**f**iliato
Pe**t**ro - **F**etero	So**p**atro - So**f**atiro	A**p**ele - A**f**ele **P**ersisi -
Fili**p**o - Fili**f**o	**P**orkio - **F**orikio	**Ferisisi**
Pilato - **F**ilato	Agri**p**a - Agiri**f**a	**Pa**troba - **Fu**tiroba
Prokono - **F**urokoni	**P**ublio - **F**ubulio	E**p**afra - E**f**af**u**ra
Parmena - **F**arimena	**P**riska -	A**p**olo - A**f**olo
Prisila -	**F**riska/**F**iriskila	Arki**p**o - Arki**f**o
Firisikila/Firisikia	E**p**aineto - E**f**aineto	A**p**olioni - A**f**olioni

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Data Na. 4

Yane - **J**anesi
Yambre – **J**amburisi
Ben**y**amini - Ben**j**ameni

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Data Na. 3 na 4 zinaonesha mabadiliko ya sauti /p/ kwenda /f/ na /Ɉ/ kuwa /y/ kutoka Kiswahili kwenda Gı̣rı̣mi, kwa mfuatano huo. /p/ ni kipasuo sighuna cha midomo na /f/ ni kikwamizi sighuna cha midomo-meno. Katika Gı̣rı̣mi, sauti /p/ na /f/ ni alofoni. Sauti /p/ hutokea katika mazingira ya kutanguliwa na kipasuo cha midomo /m/, na sauti /f/ hutokea katika mazingira ya kutotanguliwa na kipasuo hicho (Olson, 1964). Hata hivyo, tunaona /p/ katika jina la Kiswahili “Ampliato” imebadilika kuwa /f/ katika neno la Gı̣rı̣mi “Amfiliato” ingawa imetanguliwa na kipasuo /m/. Hii ni kinyume na kanuni za mfuatano wa nazali ya mdomo /m/ kutangulia kipasuo cha midomo /p/ kama anavyoeleza (Olson, 1964). Neno hilo lilipaswa kutafsiriwa kama Amụfiliato au Ampiliato katika Gı̣rı̣mi, ambapo irabu /i/ ingechopekwa baada ya kipasuo /p/ kuunda silabi huru mpi ili kukidhi mahitaji ya lugha za Kibantu.

Aidha, Sauti /Ɉ/ inabadilishwa kwa /j/ kwa sababu wazungumzaji wa LL wanapendelea zaidi sauti ya pili kuliko ya kwanza. Hata hivyo, sauti zote—/Ɉ/ na /j/—ni za kaakaa gumu, lakini ya kwanza ni kipasuo kwamizi na ya pili ni kiyeyusho. Hafez (1996) anaeleza kuwa sauti za LC zinaweza kubadilishwa kwa sauti za LL kwa upendeleo tu wa sauti fulani dhidi ya sauti nyingine bila hata sababu za kisayansi.

Kwa mujibu wa makala hii, mabadiliko mengine ya sauti yanayotokea katika tafsiri ya majina ya pekee ya watu Gı̣rı̣mi ni yale yanayohusu sauti zisizopatikana katika Gı̣rı̣mi. Kutokana na kutokuwapo kwa sauti hizo, tafsiri inatumia sauti mbadala za Gı̣rı̣mi, ambapo sauti /ɵ/ huwa /t/, na /z/ na /ʃ/ huwa /s/. Mabadiliko hayo yanawasilishwa katika Data Na. 5, 6, na 7, mtawalia.

Data Na. 5

Yo**th**amu - Yo**t**amu Bar**th**olomayo - Bari**t**olomayo **Th**adayo - **T**adayo Abia**th**ari - Abia**t**ari	**Th**eofilo - **T**eofilo Ru**th**u - Ru**t**i Me**th**usela - Me**t**usela Se**th**i - Se**t**i Mar**th**a - Mari**t**a	Ma**th**iya - Ma**t**iasi Tabi**th**a - Tabi**t**a Sos**th**ene - Sosi**t**ene Yef**th**a - Yefu**t**

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Data Na. 6

Zera - **S**era Boa**z**i - Boa**s**i U**z**ia - U**s**ia Aha**z**i - Aha**s**i He**z**ekia - He**s**ekia **Z**erubabeli - **S**erubabeli A**z**ori - A**s**ori	Mna**z**orayo - Mna**s**orayo **Z**ebedayo - **S**ebadayo **Z**akaria - **S**akaria **Z**erubabeli - **S**erubabeli La**z**aro - La**s**aro **Z**akayo - **S**akayo	**Z**ebadayo - **S**ebadayo Zeleto - **S**elote **Z**ena - **S**ena Melki**z**edeki - Meliki**s**edeki Ye**z**ebeli - Ye**s**ebeli **Z**abuloni - **S**abuloni

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Data Na. 7

Na**sh**oni - Na**s**oni A**sh**eri - A**s**eri	Yo**sh**ua - Yo**s**ua Eno**sh**i - Eno**s**i	Yeho**sh**afati - Yeho**s**afati

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Wanaisimu wanadai kuwa sauti zinazobadilishana nafasi ni zile zinazochangia sifa za kifonetiki ambazo ni mahali na namna ya matamshi pamoja na hali ya ughuna (Msuya & Mreta, 2019). Sauti /ɵ/ ni kikwamizi cha meno na /t/ ni kipasuo cha ufizi. Sauti zote zinatamkwa pasipo na mtetemo wa nyuzi sauti. Kwa hiyo, zinachangia sifa ya usighuna. Sauti /z/ na /s/ zote ni vikwamizi; cha kwanza ni ghuna na kingine sighuna. Sauti /s/ na /ʃ/ zote ni vikwamizi, /s/ ni ya ufizi na /ʃ/ ni ya kaakaa gumu. Mabadiliko ya sauti /ʃ/ na /z/ kuwa /s/ pia ni dhahiri katika lugha zingine kama vile Dholuo (Omondi, 2008). Ni jambo la kawaida kwa sauti kadhaa za LC kutafsiriwa kwa sauti moja ya LL. Jambo hili linatokana na LL kushindwa kuzitofautisha sauti hizo katika matamshi. Mathalani, Nichols (1996) anadai kuwa, katika Kigiriki, sauti /s/ na /ʃ/ hazitofautishwi kimatamshi.

Aidha, sauti /r/ na /l/ zinaonekana kutumika kwa kubadilishana nafasi. Hili limejitokeza katika tafsiri ya majina "Nafta**l**i - Naf**u**tali/Nafuta**r**i" na "Gabrieli - Gabrieli (Gabureri)". Majina ambayo yapo katika mabanomraba hayamo katika kitabu teule, ila yalitajwa na wasailiwa kwamba ndivyo yanavyotamkwa katika Gɪrɪmi. Majina haya yanaonesha kuwa sauti zote, /l/ na /r/, zipo na zinakubalika katika Gɪrɪmi. Hivyo, kwa baadhi ya maneno, zinaweza kutumika kwa mbadilishano. Kiplimo na Mwita (2021) wanadai kuwa fonimu /r/ na /l/ ni sauti zilizo na tabia sawa kwa sababu zina sifa bainifu zinazokaribiana. /l/ ni kitambaza cha ufizi ambacho hutamkwa kwa kutandaza ulimi huku ncha ya ulimi ikigusana na ufizi na kuruhusu hewa kupita pembeni mwa ulimi ambamo mna nafasi wazi. /r/ ni kimadende cha ufizi ambacho hutamkwa wakati ncha ya ulimi ikipiga ulimi harakaharaka kwenye ufizi huku hewa ikitoka nje kupitia chemba cha kinywa. Kwa hiyo, sauti hizi, katika lugha nyingi za Kibantu, hubadilishana nafasi katika maneno pasipo kuathiri maana ya maneno hayo.

Uongezaji wa sauti

Uongezaji wa sauti unahusu kuchopeka sauti ambayo haikuwapo katika neno la LC katika neno tafsiriwa la LL. Uongezaji wa sauti katika tafsiri ya Kiswahili kwenda Gɪrɪmi hujumuisha sauti za aina zote mbili ambazo ni konsonanti na irabu kama ilivyo katika lugha zingine, ikiwamo Chasu (Msuya & Mreta, 2019). Makala inaonesha zaidi kuwa lengo la kuongeza sauti ni kurahisisha matamshi ya wazungumzaji wa LL.

Uongezaji wa konsonanti

Katika kutafsiri majina ya pekee ya watu kutoka Kiswahili kwenda Gɪrɪmi, kuna uongezaji wa sauti /h/ mwanzoni mwa baadhi ya majina yanayoanza na irabu /e/ ili kurahisisha matamshi ya majina husika. Uchopekaji huu

umefanyika katika mazingira ya makutano ya sauti za aina mbili tofauti, ambapo sauti ya mwanzo ya jina ni irabu na sauti iliyopachikwa ni konsonanti. Majina ya pekee yaliyoongezewa sauti /h/ yapo katika Data Na. 8.

Data Na. 8

Esromu - **H**esironi
Eli - **H**eli
Esli - **H**esili

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Uchopekaji wa konsonanti katika Gịrịmi unahusisha sauti /h/ ambayo inachopekwa kwa maneno machache yanayoanza na irabu /e/. Katika maneno mengi ya Kibantu, uchopekaji wa sauti hii hutokea zaidi mwanzoni mwa neno, hasa kwa maneno yanayoanza kwa irabu, ingawa huweza kutokea hata katikati ya neno kabla ya silabi inayoundwa na irabu pekee (Ontieri, 2015; Nyagah, 2016). Jambo hili linanasibishwa na mazoea ya wazungumzaji wa LL kuambatisha irabu zote na sauti /h/ katika utamkaji. Akitoa mfano, Kijida[4] anasema: "Kuna majina mengi tu ambayo Waswahili huyatamka yakianza na irabu, lakini wenyeji (Arịmi/Wanyaturu) huyatamka kwa kuanza na sauti /h/. Mfano wake ni Ali (Hali) na Ogha (Hogha/Hugha)."

Kwa mujibu wa Ontieri (2015), katika lugha za Kibantu, uchopekaji wa sauti /h/ hufanyika zaidi mwanzoni mwa maneno yanayoanza kwa irabu, ambapo sababu kubwa ya kufanya hivyo ni mazoea ya matamshi ya wazungumzaji wa LL yaliyojengwa kutamka silabi zenye konsonanti na irabu (KI). Kwa ujumla, uchopekaji wa konsonanti katika utohozi ni zoezi

[4] Mahojiano baina ya mtafiti na mtafitiwa aitwaye Hawa Kijida yalifanyika tarehe 12/09/2023 katika Kijiji cha Mwakichenche.

ambalo halijazoeleka sana ikilinganishwa na udondoshwaji wake. Msuya & Mreta (2019) wanaonesha uchopekaji wa kiyeyusho /j/, na vilainisho (kitambaza /l/ na kimadende /r/) katika utohozi wa maneno kutoka Kiswahili kwenda Chasu. Hata hivyo, uchopekaji wa vilainisho katika Chasu ni rejesho la sauti za aina hiyo za Mamebantu ambazo zimedondoshwa katika maneno zilimokuwapo hapo awali (Kiplimo na Mwita, 2021).

Uongezaji wa irabu

Uongezaji wa irabu, kwa mujibu wa makala hii, ni uchopekaji wa irabu katika neno la LL wakati irabu hiyo haikuwapo katika neno la LC. Katika tathmini ya tafsiri ya majina ya pekee ya watu kutoka Kiswahili kwenda Gịrịmi, baadhi ya irabu huchopekwa. Irabu hizo ni /u/ /i/ na /e/. Irabu hizo huchopekwa kulingana na msikiko wa irabu katika silabi funge ya Kiswahili wakati wa kutamka majina. Data Na. 9, 10 na 11 zinaonesha uchopekaji wa irabu hizo.

Data Na. 9

Ibrahimu - Ib**u**rahimu Mnazorayo - M**u**na**s**orayo Prokono - F**u**rokoni **Y**ambre - **J**amburisi	Trofimo - T**u**rofimo Drusila - D**u**rusila **P**ublio - **F**ubulio **Pa**troba - **Futi**roba E**p**afra - E**f**af**u**ra	Karpo - Kari**p**usi Klaudia - K**u**laudia Naft**al**i - Naf**u**tali/Nafuta**r**i

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Data Na. 10

Esromu - Hes**i**roni Salmoni - Sal**i**moni Bartholomayo - Bar**i**tolomayo Alfayo - Al**i**fayo Magdalene - Mag**i**dalene Marko - Mar**i**ko	Simoni - Sim**i**oni Barnaba - Bar**i**naba Herme - Her**i**ma Prisila - F**i**risikila/F**i**risikia/F**i**risikila Klaudio - K**i**laudio Sosthene - Sos**i**tene Demetrio - Demet**i**rio	Priska - F**i**r**i**skila Trifaina - T**i**rifaina Trifoso - T**i**rifoso Persisi - Fer**i**sisi Asinkrito - Asink**i**rito Flegoni - F**i**legon Patroba - Fut**i**roba Stefana - S**i**tefana

Esli - Hes**i**li Arfaksadi - Arifok**i**sadi Mar**th**a - Mar**it**a Kleopa - K**i**liopa Barsaba - Bar**i**saba Yusto - Yus**i**to Parmena - Far**i**mena	Artemi - Ar**i**temi Aristarko - Aris**i**tar**i**ko Sopatro - Sofat**i**ro Porkio - For**i**kio Festo - Fes**i**to Agripa - Ag**i**rifa Bernike - Ber**i**nike Israeli - Is**i**raeli	Fortunato - For**i**tunato Hermogene - He**r**imogene Arkipo - Ar**i**kifo Diotrefe - Diot**i**refe Dorkasi - Dor**i**kasi

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Data Na. 11

Petro - Fet**e**ro Andrea - And**e**rea Stefano - S**e**tefano

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Data Na. 9 - 11 zinaonesha upachikaji wa irabu katika majina ya pekee ya watu ya Gịrịmi. Uchopekaji huu unafanyika kwa lengo la kurahisisha matamshi na kukidhi matakwa ya lugha za Kibantu ya kuwa na silabi huru yenye konsonanti na irabu (KI) (Iribemwangi, 2010). Kishe (2016) anadai kuwa kanuni ya msingi inayotumika kuasilisha majina ya lugha moja kwenda nyingine ni kuyaandika majina hayo kama yanavyotamkwa katika LC. Matamshi ya LC ndiyo yanatumika sana kutafsiri kuliko mikakati mingine (Okal, 2012, Kishe, 2016; Aubakir na Makhpirov, 2019; Valixon, 2020). Baadhi ya maneno yanapotafsiriwa, muundo wa silabi wa LL unapaswa kuzingatiwa, ambapo irabu huchopekwa ili kuunda silabi huru inayokidhi matakwa ya kanuni za LL (Okal, 2012).

Kishe (*ameshatajwa*) anafafanua kwamba uchopekaji wa irabu hufanyika pale mpangilio wa konsonanti unapokiuka kaida za LL hata kusababisha ugumu wa kugawa maneno katika silabi zinazotakiwa kutamkika kiasili. Anaendelea kufafanua kwamba kanuni hii hurekebisha mifululizo ya

konsonanti isiyokubalika kwa kuchomeka irabu. Madhumuni yake ni kuondoa mfuatano wa konsonanti ili kulingana na utaratibu wa LL wa konsonanti kufuatiwa na irabu, yaani CVCV, kwa maana ya kuepuka silabi funge.

Udondoshaji wa sauti

Katika tafsiri, udondoshaji wa sauti ni kitendo cha kuacha sauti fulani iliyokuwapo kwenye neno la LC wakati wa kulihawilisha kwenda L kwa lengo la kutii sarufi ya LL (Msuya & Mreta, 2019). Katika tafsiri ya majina ya pekee ya watu kutoka Kiswahili kwenda Gɪrɪmi, baadhi ya sauti zinaachwa ili kurekebisha matamshi ya majina hayo na kuzingatia muundo wa sarufi ya LL. Kuna udondoshaji wa sauti /h/ ambayo ni kikwamizi ghuna cha glota pale inapotokea mwanzoni mwa neno na kufuatiwa na sauti /a/. Udondoshaji huo umejitokeza katika tafsiri ya majina yanayowasilishwa katika Data Na. 12.

Data Na. 12

Har**u**ni - Ar**o**ni/Aaroni
Habili - Abeli
Henoko - Enoki

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Katika Data Na. 8, tumeona sauti /h/ inadondoshwa katika tafsiri ya majina ya pekee yanayoanza kwa irabu /e/. Hali ni kinyume na Data Na. 12, ambapo kuna udondoshaji wa sauti /h/ katika majina yanayoanza na irabu, hasa /a/ na /e/. Nyagah (2016) anadai kwamba huu ni usahilishaji kwa sababu utamkaji wa irabu pekee kama silabi huwa rahisi ikilinganishwa na utamkaji wa silabi ya konsonanti /h/ na irabu. Pamoja na utetezi huu wa Nyagah (*keshatajwa*), bado kuna mkanganyiko katika udondoshaji na uchopekaji wa sauti /h/ kabla ya irabu, hususani kwa nomino zinazoanza na

irabu /e/. Kwa nini wakati mwingine ichopekwe na kwa nini wakati mwingine idondoshwe? Majibu ya utafiti yanaonesha kuwa wazungumzaji wengi wa lugha za Kibantu huweza kutamka irabu kwa kuziambatisha na sauti /h/ na wengine hutamka irabu bila kuweka sauti hiyo.

Kadhalika, imeonekana kuwa kuna udondoshaji wa sauti /r/ katika baadhi ya majina ya Kiswahili yanapohawilishwa katika Gɪrɪ̣mi. Utafiti umeonesha kuwa msikiko wa sauti hiyo inapoambatana na konsonanti nyingine unakuwa hafifu ndio maana ni rahisi kudondoshwa na wazungumzaji wa LL. Mifano ya maneno ambayo sauti /r/ imedondoshwa ipo katika Data Na. 13.

Data Na. 13

Boane**r**ge - Boanege
A**r**tema - Atema

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Konsonanti /r/ inadondoshwa katika mazingira ya kufuatwa na konsonanti nyingine. Ngowa (2015) anafafanua kuwa udondoshaji wa sauti hii unalenga kuvunja muundo mfululizo wa konsonanti za nomino za LC na kutengeneza silabi huru ya konsonanti + irabu ya LL. Hata hivyo, data hii ni ndogo kuhitimisha na kuthibitisha kuhusu udondoshwaji wa sauti /r/ katika utohozi wa majina ya pekee ya watu kutoka Kiswahili kwenda Gɪ̣rɪ̣mi.

Upungufu Uliojitokeza katika Tafsiri

Pamoja na ubora wa tafsiri ya majina ya pekee kutoka *Agano Jipya* kwa Kiswahili kwenda katika Gɪ̣rɪ̣mi ambao umechangiwa na mikakati iliyotumika, kuna upungufu katika tafsiri ya majina hayo pia. Upungufu huo unatokana na ubadilishaji wa sauti usiotabirika, tafsiri kuegemea zaidi

katika Kiingereza badala ya Kiswahili ambayo ni LC, na jina moja kutafsiriwa kwa ruwaza mbili tofauti au zaidi.

Ubadilishaji wa sauti usiotabirika

Katika tafsiri ya majina ya pekee ya watu kutoka *Agano Jipya* la Kiswahili kwenda Gɪrɪ̣mi, kuna ubadilishaji wa sauti usiotabirika. Ubadilishaji huu umejitokeza zaidi katika irabu. Data Na. 14 inawasilisha majina hayo yenye mabadiliko ya irabu yasiyotabirika.

Data Na. 14

Aram**u** - Ram**i** (/u/ > /i/)
Elm**a**damu - El**i**m**o**damu (/a/ > /o/)
Nik**o**lao - Nik**a**lao (/o/ > /a/)
L**i**sia - L**u**sia (/i/ > /u/)
Her**i**dioni - Her**e**dioni (/i/ > /e/)
Barak**a** - Barak**i** (/a/ > /i/)
Isaka - Isaki (/a/ > /i/).

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Mabadiliko ya fonimu za irabu katika Data Na. 14 yanaonekana kutokuwa thabiti na yanatokea katika majina machache, yaani katika jina moja au mawili tu. Kulingana na utokeaji wa kiasi kidogo na utothabiti huo, ni vigumu kujumuisha na kuhitimisha kuhusu mabadiliko yanayotokea katika uhawilishaji wa majina hayo.

Tafsiri kulandana zaidi na majina ya Kiingereza

Matini za kidini ni za kitamaduni. Kwa hiyo, ni tafsiri hifadhi au tafsiri rejelezi ambazo humruhusu mfasiri kurejelea MC ya/za mwanzo, yaani zilizotumika kuandaa MC ambayo imezalisha ML inayoshughulikiwa.

Kupitia usaili, mmoja wa wafasiri wa *Agano Jipya* kutoka Kiswahili kwenda Gịrịmi[5] anayakinisha hoja hii kwa kusema:

> Kiswahili kilitumika kama MC kuandaa tafsiri hiyo, lakini, wakati mwingine, sisi wafasiri tulirejelea *King James Version* na *Revised Standard Version* (RVS). Lengo la kurejelea matoleo hayo ya biblia lilikuwa kupata uelewa zaidi wa vipengele ambavyo havikueleweka vizuri kwenye matini ya Kiswahili, hasa vya kimaudhui. Kwa hiyo, wakati wa kuhawilisha maudhui, tulijikuta wakitohoa majina ya pekee ya watu moja kwa moja kutoka Kiingereza kwenda katika Gịrịmi.

Majina katika Data Na. 15 ndiyo yaliyotoholewa moja kwa moja kutoka Kingereza.

Data Na. 15

Sulemani - Solomoni (Solomon)	Sosthene - Sostenes (Sosthenes)	Yambre - Jamburisi (Jambres)	
Yusufu - Yosefu (Joseph)	Iskanda - Alekisanda (Alexander)	Kreske - Kireseni (Crescens)	
Eri - Evi (Levi)	Feliki -Felikisi (Felix)	Karpo - Karipusi (Carpus)	
Nuhu - Noa (Noah)	Flegoni - Filegon (Phlegon)	Haruni - Aroni/Aaroni (Aaron)	
Lutu - Loti (Lot)	Hawa - Eva (Eve)		
Mathiya - Matiasi (Matthias)	Damari - Damarisi (Damaris)		
Yane - Janesi (Jannes)	Ayubu - Yobu (Job)		
Piro - Firiho (Pyrrhus)			

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Majina ya pekee ya watu waliyotafsiriwa, kama yanavyoonekana katika Data Na. 15, yamekuwa tofauti kidogo na yale ya Kiswahili ambayo ndiyo ilikuwa MC mama. Jambo hili linasababisha wasomaji wa ML ambao wamebahatika kusoma MC ya Kiswahili kupata mkanganyiko na

[5]Mtafitiwa ambaye ni mchungaji mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kati (Singida) hakutaka jina lake litajwe. Mahojiano kati yake na mtafiti yalifanyika tarehe 22/09/2023 kwa njia ya arafa za *WhatsApp*.

kushindwa kuiamini tafsiri ambayo imetokana na matini ya Kiingereza. Pamoja na kufuatilia maudhui katika matini ya Kiingereza kama ilivyoolezwa na mmoja wa wafasiri, wafasiri walipaswa kuzingatia na kuwianisha majina ya matini ya Kiswahili ambayo ilikuwa MC mama na ML ya Gịrịmi.

Majina kutafsiriwa kwa ruwaza zaidi ya moja

Kutafsiri elementi moja kwa namna mbili au zaidi tofauti huweza kumpotosha msomaji wa matini lengwa (Stephano & Gwajekera, 2019). Katika tathmini iliyofanyika, majina ya pekee ya watu yamedhihirika kutafsiriwa kwa ruwaza mbili au zaidi na kuonekana kama majina ya watu tofauti. Majina hayo yanawasilishwa katika Data Na. 16, ambapo yametenganishwa kwa alama ya mkwaju (/). Katika mabano ni vifungu vya mistari ya *Agano Jipya* kwa Gịrịmi inayoonesha tafsiri hizo tofauti.

Data Na. 16

Ibrahimu - Iburahamu/Iburahimu (Matayo1:17; Matayo 22:32; Mariko12:26)
Simoni - Simoni/Simioni (Mariko14:3; Luka 5:5; Ntendo 10:5)
Zebedayo - Zebedayo/Sebadayo (Matayo 4:21; Matayo 27:56; Mariko1:19)
Filipo - Filipo/Filifo (Matayo 10:3; Ntendo 8:5; Yohana 12:21, 22; Yohana1:44; Ntendo 8:13, 30, 35)
Eliya - Elia/Eliya (Matayo 11:14; Luka 9:30, 33; Matayo 17:3, 11; Mariko 9:4, 11, 12; Yakobo 5:17)
Mariamu - Mariamu/Maria (Mathayo1:16; Mariko16:9)
Zakaria - Sakaria/Zakaria (Luka 1:13; Luka 1:59)
Haruni - Aroni/Aaroni (Luka 1:5; Aeburania 5:4)
Isaka - Isaka/Isaki (Matayo1:2; Eburania 11:7, 9; Arumi 9:7; Agalatia 4:28; Yakobo 22:21)
Prisila - Firisikila/Firisikia (Ntendo 18:2, 18, 26)
Sosthene - Sositene/Sostenes (Ntendo 18:17; 1 Akorinto 1:1)
Priska - Friska/Firiskila/Pirisika (I Akorinto16:19; 2; Timoteo 4:19)
Stefana - Sitefana/Stefana (1Akorinto 1:16; 1 Akorinto 16:15)
Silwano - Silwano/Silasi (2 Akorinto1:19; 1 Atesalonike1:1; 2 Atesalonike1:1; 1Fetero 5:12)

Naftali - Nafutali/Nafutari (Matayo 4:15; Ufunuo 7:6) Zabuloni - Zabuloni/Sabuloni (Matayo 4:15; Ukunukuo 7:8)

Chanzo (Data za Utafiti, 2023)

Katika Data Na. 16, majina yametafsiriwa kwa namna tofautitofauti, yaani jina moja limetafsiriwa kwa ruwaza mbili au zaidi. Tofauti hizo zimetokana na ama kubadilishwa kwa sauti, kuhifadhi sauti ya mwanzo, kuchopeka, au kudondosha sauti katika majina yanayomrejelea mtu mmoja. Tafsiri hizi zinasababisha mkanganyiko kwa wasomaji wa tafsiri lengwa na kushindwa kuelewa kama ni jina la mtu mmoja au watu wengi wanaorejelewa kwa majina tofauti. Suala la kukosekana kwa urari katika tafsiri ya majina ya pekee ya watu linajitokeza katika tafsiri nyingi za matini teule. Inabidi kuwa na kigezo kimoja maalumu kinachozingatia mazingira ya wasomaji lengwa tunapotafsiri majina ya pekee ili kuwa na ulinganifu na kuondoa mkanganyiko kwa wasomaji kama anavyoeleza Rodríguez (2003).

Hitimisho

Tathmini ya tafsiri ya majina ya pekee ya watu kutoka Kiswahili kwenda Gɪrɪ̣mi imeonesha kuwa mikakati inayopendelewa ni unakilishaji na utohozi wa majina. Kulingana na Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano, mikakati hii miwili imedhihirika kuwa mwafaka katika kuyahifadhi majina kutoka LC ambayo yamebeba ujumbe, maudhui na hisia za visa vya kibiblia. Aidha, makala imeonesha kuwa, pamoja na mikakati hiyo faafu kutumika, bado kuna upungufu katika tafsiri hizo. Upungufu huu unachangiwa na tafsiri ya LL kuegemea katika Kiingereza badala ya Kiswahili ambayo ni LC, utothabiti wa kutafsiri majina hayo na ukiukaji wa kanuni za lugha lengwa. Kufuatia matokeo haya, makala inapendekeza mambo matatu yanayoweza kuchangia ufanisi katika tafsiri ya majina ya pekee ya watu kutoka lugha moja kwenda nyingine. Mosi, mikakati faafu

iendelee kutumika ili kuzalisha tafsiri bora. Pili, wafasiri wazingatie MC mama wanapotafsiri majina ya pekee ya watu ili kuwa na uwiano wa majina hayo baina ya MC na ML. Tatu, wafasiri wazingatie kaida za LL na urari katika kutafsiri majina ya pekee kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine.

Marejeleo

Aubakir, N., & Makhpirov, V. (2019). Towards the Issue of Translating Proper Names on the Materials of National Geographic Magazine Proceedings of INTCESS. 6th *International Conference on Education and Sociak Scinces, 4 - 6 February 2019 - Dubai. U.A.E.*

Dweik, B., & Al-Sayyed, S. (2016). Translating Proper Nouns from Arabic into English: Barries and Procedures. *Arab World English Journal (AWEJ)*, Special Issue on Translation (5), 181-194.

Halimal, A. (2016). Translating Arabic Proper Names: A Foreignising Approach. *Internation Journal of English Language and Linguistics Research*, 4(2), 1-16.

Iribemwangi, P. (2010). *The Structure of Swahili: Sounds, Sound Changes and Words.* Saarbrucken: VDM Verlag.

Issa, I. (2017). Mistranslation of Prophets' Names in the Holy Quran: A Critical Evaluation of Two Translations. *Journal of Education and Practice*, 8(2), 168-174.

Kiplimo, C., & Mwita, L. (2021). Thibitisho la Udondoshaji wa Kihistoria wa Fonimu za Likwidi. *East Africa Journal of Swahili Studies*, 4(1), 43-46.

Kishe, A. (2016). Kuingiliana kwa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza: Uswahilishaji wa Maneno ya Kiingereza. *Huria Journal*, 2(1), 91-105.

Msuya, J., & Mreta, A. (2019). Adaptation of Loan Words in Chasu. *Journal of Linguistics and Language in Education*, 13(1), 26-46.

Naumova, K. (2014). Legal Aspects of Transcription of Personal Names in the Latvian Language. *Riga Graduate School of Law (RGSL), Research Paper No.11*.

Ngowa, N. (2015). *Uchanganuzi wa Nomino-mkopo za Kigryama kutoka Kiingereza* (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Pwani, Kilifi.

Nichols, A. (1996). *Translating the Bible: A Critical Analysisi of E.A. NIDA's Theory of Dynamic Equivalence and its Impact Upon Recent Bible Translations* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Sheffield, United Kingdom.

Nyagah, S. (2016). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia na Kimofolojia Yanayojitokeza katika Kazi Andishi za Wanafunzi wa Shule za Upili, Tigania, Jimbo la Meru* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Okal, B. (2012). Nafasi ya Tafsiri katika Taaluma ya Onomastiki: Uhakiki wa Mbinu Zake katika Tafsiri ya Toponomastiki. *Kiswahili*, 75, 27-42.

Olson, H. (1964). *The Phonology and Morphology of Rimi.* Connecticut: Hartford Studies in Linguistics.

Omondi, O. (2008). *Utohozi Fonolojia wa Maneno-mkopo ya Dholuo kutoka Kiswahili* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Ontieri, J. (2015). Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kwanza katika Kiswahili: Mfano wa Lugha Teule za Kibantu nchini Kenya. *Mulika*, 34, 1-13.

Rodríguez, M. (2003). The Problem of Translating Proper Names in Harry Potter and the Lord of the Rings. *ES 25*, 123-136.

Shirinzadeh, S., & Mahadi, T. (2014). Translating Proper Nouns: A Case Study of English Translation of Hafez's Lyrics. *English Language Teaching*, 7(7), 8-16.

Stephano, R., & Gwajekera, F. (2019). Ufanisi wa Tafsiri za Viwandani Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Vifungashio vya Dawa za Binadamu. *Mulika*, 38, 26-42.

Valixon, A. (2020). Proper Names in the Process of Translation in Terms of English and Russian Languages. *International Journal of Academic Pedagogical Research (IJAPR)*, 4(10), 21-23.

Winford, D. (2003). *A Introduction to Contact Linguistics.* Oxford: Blackwell.